**HOTUBA YA WAKILI MKUU WA SERIKALI DKT. BONIPHACE NALIJA LUHENDE, KATIKA KIKAO CHA PILI CHA BARAZA LA PILI LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024, KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA NSSF, MKOANI MOROGORO 19 APRILI, 2024**

**Mhe. Jumanne Sagini (Mb.), Naibu Waziri wa Katiba na Sheria,**

**Bw. Mark Mulwambo, Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Alice Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Mteule; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Zuhura Kussaga, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Stanley Mahenge, Naibu Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mtani Songorwa, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Sarah Rwezaula, Katibu wa TUGHE Ngazi ya Mkoa Dar es Salaam;**

**Bw. Nsubisi Mwasandenge, Mwakilishi wa TUGHE Taifa;**

**Viongozi wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Ndg. Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana,**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, SOLIDARIIIIIITY;**

**MSHIKAMANOOO.**

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu rahimu mwingi wa Rehema na Fadhila kwa kutufikisha siku hii ya leo tukiwa na afya njema. Pili, napenda kutumia fursa hii kuwakaribisha wote katika Mkutano wa Pili wa Baraza la Pili la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwako kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. Mimi binafsi na Ofisi nzima ya Wakili Mkuu wa Serikali tunaahidi kukupa ushirikiano na kufanya kazi bega kwa bega kwa maendeleo ya taifa letu. **Hongera sana Mhe. Naibu Waziri**

Pamoja na hayo, napenda kukushukuru sana kwa kutenga muda wako na kuweza kuhudhuria katika Baraza hili. Natambua una majukumu mengi sana lakini umekubali ombi letu na kuweza kujumuika nasi leo hii. Kufika kwako ni ishara muhimu kwetu na inaonesha ushirikiano wako na Ofisi hii ambayo ni sehemu ya Taasisi zilizochini ya Wizara yako. **Asante sana.**

**Mhe. Mgeni Rasmi**;

Naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza **Bi. Alice Mtulo** kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, uteuzi huu umeonyesha ni namna gani Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa tanuru la kuandaa viongozi makini kwa maslahi mapana ya Taifa. **Hongera Sana. Bi Mtulo. Nakutakia kila la Kheri katika Utekelezaji wa Majukumu yako mapya.**

**Mhe. Mgeni Rasmi;**

Kipekee napenda kumshukuru sana **Bw. Mark Mulwambo**, Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, kwa kutekeleza majukumu ya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha takribani miezi saba (7) toka **Bi. Sarah Mwaipopo** aliyekuwa NWMS kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Jaji wa Mahakama Kuu. Aidha namshukuru **Bw. Mulwambo** kushirikiana kikamilifu na Viongozi wa Baraza la Wafanyakazi katika kusimamia maandalizi ya Baraza hili. Napenda pia kuwashukuru wale wote

walioshiriki kufanikisha maandalizi ya Mkutano huu muhimu ***'Hongereni Sana''*.**

Vile vile, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe kutoka TUGHE Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kufanya kazi kwa karibu na Tawi la TUGHE la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha Baraza hili la Wafanyakazi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria na kanuni.

**Mhe. Mgeni Rasmi;**

Mwaka huu tulimpoteza Mfanyakazi Mwenzetu, aliyekuwa Wakili wa Serikali Mfawidhi Mkoa wa Shinyanga, Bw. Solomoni Lwenge aliyefariki ghafla nyumbani kwake Shinyanga mwezi wa pili. Hivyo naomba tutumie nafasi hii kumkumbuka kwa kusimama kwa utulivu kwa dakika moja na tuendelee kumwombea Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi. **AMEN!**

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Hiki ni Kikao cha Pili cha Baraza la Pili la Wafanyakazi katika OWMS kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024**. Kama alivyoeleza Makamu Mwenyekiti, kikao hiki ni utekelezaji wa takwa la kisheria la kuwashirikisha Wafanyakazi katika Uongozi wa Pamoja Mahala pa Kazi, kwa mujibu wa Kanuni Na. 108 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2003, vile vile, Kifungu cha 73 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya

Mwaka 2004 na Kifungu cha 30 (3) cha Sheria ya Majadiliano ya pamoja na Kanuni Na. 24 ya Kanuni za Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2005.

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

OWMS ilianzishwa tarehe 13 Februari, 2018 na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Tangazo la Serikali Na. 50/ 2018 ikiwa na jukumu la kuratibu, kusimamia, kushauri na kuendesha Mashauri yote ya Madai na Usuluhishi yanayofunguliwa dhidi au kwa niaba ya Serikali na Taasisi zake ndani na nje ya Nchi.

Uwepo wa Baraza la Wafanyakazi ndani ya OWMS umekuwa na manufaa makubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Baraza la wafanyakazi limeamsha ari ya uchapakazi kwa watumishi na kuboresha ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika majukumu ya kila siku ya Ofisi hii, hivyo kupelekea mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka sita tu tangu kuanzishwa kwake.

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha mashauri **7992** (yaani mashauri **7813** ya madai na **179** ya usuluhishi).

Katika kuendesha mashauri **7813** ya madai, mashauri **762** yalimalizika.

Aidha, kati ya mashauri ya madai yaliyomalizika, mashauri **719** yalihitimishwa kwa njia ya kimahakama na mashauri **43** yalihitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya mahakama.

Kwa kipindi tajwa, OWMS ilishinda jumla ya mashauri **705** yenye madai ya fedha na kufanikiwa kuokoa fedha za Serikali jumla ya Shilingi **3,474,067,009,683.45** (Trilioni 3.47) ambazo zingelipwa iwapo serikali ingeshindwa mashauri hayo. Vilevile Ofisi imeokoa jumla ya Shilingi 10,205,263,509.43 (Bilioni 10.2) zilizotokana na mashauri 43 yaliyohitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama. Hivyo Ofisi imeokoa jumla ya Shilingi **3,484,272,273,192.88 (Trilioni 3.48)** kwa kushinda kesi na majadiliano.

Hata hivyo katika kipindi husika, Ofisi imeshindwa jumla ya mashauri ya madai 14 yenye madai ya fedha na kupoteza jumla ya Shilingi **1,259,249,021.00 (Bilioni 1.25).** Hivi sasa, OWMS inaendelea kuendesha mashauri ya madai 7,051 katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Kwa upande wa mashauri ya usuluhishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi **179**. Katika kuendesha na kushughulikia mashauri hayo, jumla ya mashauri **18** yalimalizika**,** ambapo

mashauri **8** yalimalizika kwa njia ya mabaraza/mahakama ndani ya nchi na mashauri **2** yalimalizika kwa njia ya mabaraza nje ya nchi. Aidha mashauri **2** ya kitaifa na mashauri **6** ya kimataifa yalimalizika kwa njia ya majadiliano.

OWMS imewezesha Serikali kushinda katika mashauri matano (5) ya usuluhishi yaliyoendeshwa ndani ya nchi (Kitaifa) na kuokoa fedha za Serikali Shilingi 7,297,302,818.21 (**Billioni 7.2**) na Dola za Marekani 12,399,496.912 **(Millioni 12)** ambazo ni sawa na Shilingi 29,234,471,042.64. Aidha, Ofisi imewezesha Serikali kushinda shauri moja (1) la kimataifa na kufanikiwa kuokoa jumla ya Dola za Marekani 14,457,182.33 **(Takriban bilioni 36.9 za fedha za kitanzania)**

Katika kuendesha mashauri ya usuluhishi kwa niaba ya Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeendesha majadiliano ya kusuluhisha migogoro baina ya Serikali na wadaawa nje ya Mahakama ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2023/2024 hadi kufikia Aprili, 2024, mashauri nane (8) ya usuluhishi yamehitimishwa kwa njia ya majadiliano nje ya Mahakama, ambapo mashauri mawili (2) yamesuluhishwa nje ya Mahakama ndani ya nchi (Kitaifa) na mashauri sita (6) yamesuluhishwa nje ya Mahakama za kimataifa. Ambapo katika mashauri ya kitaifa Serikali imeokoa **Shilingi 47,510,903,758.35** na kwa upande wa kimataifa Serikali

imeokoa Dola za Marekani **60,322,799.82** ambazo ni sawa **Shilingi 141,456,965,577.90.** Aidha**,** katika kufanya majadiliano ya mashauri ya usuluhishi ya kitaifa na kimataifa Serikali imeokoa jumla ya **Shilingi 223,688,020,906.46.**

Hata hivyo, Serikali imeshindwa katika mashauri ya usuluhishi manne (**4**) ambapo mashauri matatu (**3**) kati ya hayo yametokana na usuluhishi kwenye vyombo na mabaraza ndani ya nchi (Kitaifa) na kupoteza kiasi cha Shilingi **1,052,201,327.20** na shauri moja (**1**) limetokana na usuluhishi kwenye vyombo na mabaraza ya usuluhishi nje ya nchi (Kimataifa) na Serikali imepoteza Dola za Marekani **110,000,000** ambayo ni sawa na **Shilingi 257,950,000,000** na kufanya Serikali kupoteza jumla ya Shilingi **259,002,201,327.20 (Billioni 259)**. Hivi sasa, OWMS inaendelea kuendesha mashauri ya usuluhishi **161** katika vyombo na mabaraza mbalimbali ya usuluhishi ndani na nje ya nchi.

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Baadhi ya mashauri ambayo OWMS imeendesha kwenye  kipindi tajwa na kupata mafanikio makubwa ni pamoja na mashauri  kwenye makundi yafuatayo;-

### i. MASHAURI YALIYOMALIZIKA KWA SERIKALI KUSHINDA MABILLIONI YA FEDHA KWENYE MAHAKAMA NA MABARAZA YA USULUHISHI NDANI NA NJE YA NCHI.

OWMS imefanikiwa kuendesha na kumaliza kwa ushindi wa mabilioni ya fedha mashauri mbalimbali ikiwemo;-

#### a. SHAURI LA USULUHISHI NA. 2682/AZO BAINA YA WAKALA WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA (PETROLEUM BULK PROCUREMENT AGENCY-PBPA) NA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI DHIDI YA KAMPUNI YA ALCHEMIST ENERGY TRADING DMCC.

Tarehe 06 Machi, 2024, Baraza la Kimataifa la Biashara (International Chamber of Commerce-ICC) lilitoa uamuzi wake na kuipa Serikali ushindi katika shauri tajwa. Shauri hili lilifunguliwa baada ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kushindwa kusambaza mafuta kwa mujibu wa Mkataba ulitokana na Zabuni ya kuleta nchini mafuta yenye Metriki za Ujazo 36,192. Katika uamuzi wake, Baraza la ICC limetamka kuwa Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC ilivunja Mkataba na kuipa Serikali ushindi wa zaidi ya **Dola za Marekani 14,457,182.33 (Takriban Tshs bilioni 36.9)**

#### b. SHAURI LA QD CONSULT LIMITED DHIDI YA PSSSF

OWMS iliendesha na kushinda shauri hili ambalo ilikuwa inadaiwa kiasi cha TZS **Billion 11.25**. Hivyo kuokoa gharama ambazo serikali ingetakiwa kulipa kama ingeshindwa shauri hilo.

**c. Mashauri mbalimbali yaliyotokana na madai ya malipo ya pensheni na kodi kwa taasisi za Serikali.**

Serikali kupitia OWMS ilifungua mashauri mbalimbali ikidai malimbikizo na madai ya Pensheni, madeni ya malipo ya umeme na kodi za upangaji. Kupitia mashauri haya  Serikali iliweza kurejeshwa mabilioni ya fedha ambazo ilikuwa inadai. Kwa mfano, kupitia shauri la madai ya malimbikizo ya kodi  lililofunguliwa na Bodi ya pamba nchini Serikali iliweza kushinda TZS. 5,184,367,455.89 **(Billioni 5.1)**. Pia kupitia shauri la TANESCO kuhusu madeni ya malipo ya Umeme na Serikali iliweza kushinda kiasi cha TZS. 205,767,807.72 **(Millioni 205. 7)** pamoja na riba.

**ii. MASHAURI MBALIMBALI YA KIKATIBA NA HAKI ZA BINADAMU YENYE MASLAHI MAPANA YA TAIFA**

**a. SHAURI LA KIKATIBA LA HUMPREY SIMON MALENGA DHIDI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (MISC. CIVIL CAUSE NO.07/2023) NA MPALE KABA MPOKI DHIDI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MWENZAKE, (MISC CIVIL CAUSE NO 11/2023)**

Mashauri ya kikatiba ya kupinga kuongezewa muda wa kustaafu wa Jaji Mkuu wa Tanzania. Mashauri haya yalitupiliwa mbali kwa mahakama kuamuru kuwa katiba ya nchi  haikuvunjwa.

**iii. MASHAURI YANAYOHUSU MIRADI MIKUBWA YA KIUWEKEZAJI NA YENYE TIJA KUBWA KWENYE MAENDELEO YA NCHI**

**a. ALPHONCE LUSAKO & 3 OTHERS VS. THE ATTORNEY GENERAL & 3 OTHERS, MISC. CIVIL CAUSE NO. 5 OF 2023; MECZEDECK MAGANYA V. THE ATTORNEY GENERAL & 2 OTHERS, MISC. CIVIL CAUSE NO 9 OF 2023; AND FREDRICK ATTORNEY MBOMA VS AG**

Serikali ilishinda mashauri yaliyofunguliwa na waleta maombi hapo juu, wakipinga utiaji saini wa Mkataba wa Uwekezaji katika bandari ya Dar es salaam. Kutokana na ushindi huo, Serikali iliendelea kutia saini mkataba huo na kuruhusu mwekezaji kuendelea na uwekezaji ambao unatarajia kuleta manufaa mbalimbali kwa watanzania wote.

**b. MAOMBI BAINA YA BARAZA LA USHINDANI DHIDI YA SCANCEM INTERNATIONAL DA, (TRIBUNAL APPLICATION NO. 16/2023)**

Tarehe 27 Oktoba, 2023, Baraza la Ushindani lilitoa ushindi kwa Serikali dhidi ya maombi ya Kampuni ya Scancem ya kuzuia muungano wa kampuni ya Simenti ya Twiga. Uwekezaji wa zaidi ya Dola Millioni 300.

***c.*** **CENTER FOR FOOD AND ADEQUATE LIVING RIGHTS AND 3 OTHERS DHIDI YA MWANASHERIA MKUU TANZANIA NA UGANDA, REFERENCE NO. 39/2020**

Tarehe 29 Novemba, 2023 Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ilitupilia mbali kesi iliyokuwa inaomba amri ya kusitisha ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki kuanzia Hoima, Uganda hadi Chongoleani Tanga, Tanzania. Thamani ya mradi huu ni wa zaidi ya fedha za kitanzania **Trillioni 4** na zaidi ya 80% ya ujenzi wa mradi huu uko Tanzania. Mradi huu unatarajia kuleta faida mbalimbali nchini ikiwemo kodi, fidia ya ardhi, kuboresha makazi ya wazawa, na kukuza uchumi.

**iv. MASHAURI YA KITAIFA NA KIMATAIFA YALIYOMALIZIKA KWA NJIA YA MAJADILIANO NA MARIDHIANO**

a. **SHAURI LA USULUHISHI BAINA YA KAMPUNI YA CRMBEG-CRCEG JV DHIDI YA MAMLAKA YA BANDARI**

Kupitia shauri hili, kampuni ya CRMBEG-CRCEG JV ilidai Mamlaka ya Bandari Tanzania zaidi ya kiasi cha TZS billion 63 kama madai yake kutokana na mkataba Na. AE/016/2015-16/CTB/W/37 wa ujenzi wa

Bandari ya Mtwara. Serikali iliweza kumaliza shauri hili kwa njia ya majadiliano na kumlipa mdai kiasi cha TZS. Billioni 15. Kutokana na kumalizika kwa shauri hilo kwa majadiliano Serikali iliweza kuokoa kiasi cha TZS. Billioni 47 ambazo zingelipwa iwapo mdai angeshinda shauri hilo.

**b. SHAURI LA USULUHISHI LA ICSID NA. ARB/20/25 BAINA YA KAMPUNI YA WINSHEAR GOLD CORP DHIDHI YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Kupitia shauri hili Kampuni ya Winshear Gold Serikali iliishtaki Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika Baraza la ICSID kufuatia Serikali kufuta Leseni Hodhi zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni hiyo, kupitia Marekebisho ya Sheria za Madini yaliyofanyika mwaka 2017 na Kanuni za Haki Madini zilizotungwa 2018. Hivyo, Kampuni iliwasilisha madai yake katika Baraza la ICSID ikiomba baraza hilo kutoa amri kuwa Serikali ya Tanzania imetaifisha uwekezaji wa Kampuni yake na kuomba kulipwa fidia ya kiasi cha Dola za Marekani **Millioni 96**. Serikali ilifanya majadiliano na kampuni hiyo na kuweza kumaliza mgogoro huo kwa kuwalipa kiasi cha **Dola za Marekani Million 30**. Hivyo kuokoa **Dola za Marekani Millioni 66** ambazo ni zaidi ya **TZS Billioni 165.**

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

Pamoja na utekelezaji wa majukumu hayo ya uendeshaji wa mashauri. OWMS pia imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mafanikio makubwa kama ifuatavyo:-

i. **Moja,** kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango ili kuhakikisha wigo wa kibajeti unaongezeka ili kuboresha mazingira ya kazi na ubora wa huduma zinazotolewa na Ofisi kwa jamii. Ambapo makadirio ya Mapendekezo ya Mpango na Bajetii kwa **Mwaka wa Fedha 2024/25** ni **Shilingi 20,750,720,000.** Tunashukuru sana Mhe. Rais kwa kutuongezea ukomo wa bajeti kutoka kiasi cha **Shilingi bilioni kumi na saba, milioni sabini na tano, laki nane na elfu hamsini (Tshs 17,075,850,000/=)**. Ambapo ongezeko la bajeti ya mwaka 2024/25 ni **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni mia sita sabini na nne, laki nane na elfu sabini (Tshs. 3,674,870,000)** sawa na ongezeko la asilimia **21.52** ikilinganishwa na Bajeti inayoendelea ya Mwaka **2023/2024.**

ii. **Mbili,** Ikama ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa sasa ni watumishi **312** Ikiwa mawakili wa Serikali **175** na watumishi wa kada nyingine ni **137.** Hadi Aprili 2024, Ofisi ina jumla ya watumishi **238**

ikiwa Mawakili wa Serikali **125,** Makatibu Sheria **18** na watumishi wa kada nyingine **95**.

iii. **Tatu,** kwa upande wa mafunzo Ofisi imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwemo mafunzo ya kiubobevu katika maeneo maalum. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 jumla ya watumishi **11** wamepatiwa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na watumishi **56** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi; na

iv. **Nne,** Ofisi inaendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, Dodoma lenye ukubwa wa mita za mraba **17,342** unaogharimu kiasi cha **Shilingi 26,740,706,111.79** ambacho kinajumuisha gharama za mkandarasi kiasi cha **Shilingi 26,242,926,061.79** na Mshauri elekezi kiasi cha **Shilingi 497,780,050.00.** Mradi umeanza kutekelezwa Julai **2022,** na hadi kufikia Machi 2024 mradi umefikia asilimia **47** ya utekelezaji wake**.**

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Ni wazi kuwa mafanikio haya na mengine mengi tunayoendelea kuyapata ni matunda ya kuwa na Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi. Kutokana na baraza hili watumishi wa OWMS wameweza kushiriki moja kwa moja

katika majukumu mbalimbali ya kitaasisi, kupitia uandaaji wa nyaraka kama vile Bajeti ya kila mwaka, Mpango kazi wa kila mwaka na Mpango Mkakati wa OWMS wa Miaka Mitano (2021/2026).

Aidha, watumishi wamepata nafasi za kuwasilisha mapendekezo, changamoto mbalimbali katika utendaji kazi wa Ofisi, na kuzitafutia ufumbuzi, kupitia vikao vya idara na Vitengo, vikao vya wafanyakazi wote pamoja na vikao vingine vya kisheria kama Baraza la wafanyakazi. Pia ofisi yetu huwa na kikao cha wafanyakazi wote kila mwaka. Kwa mwaka huu inatarajia kuwa na kikao hicho Mwezi Mei, 2024

Kama ilivyo dhumuni kuu la mkutano huu ni kuwawezesha wafanyakazi

**Mhe. Mgeni Rasmi**,

OWMS kama Ofisi ya Umma inashiriki kikamilifu kuhakikisha inatekeleza ipasavyo majukumu yake na kuhakikisha inasimamia na kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya Nchi. Katika utekelezaji wa majukumu hayo, OWMS inazingatia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo mbalimbali pamoja na Mila na Desturi zinazosimamia shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kupitia mifano ya mashauri hapo juu, tunajionea wazi kuwa OWMS inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi kwa kushiriki katika

utatuzi wa haraka wa migogoro inayohusu Serikali na Washitiri wake, Serikali na wananchi, au taasisi ili kuziwezesha pande husika kuendelea na shughuli za maendeleo. Kwa kutambua hilo OWMS imeweka mikakati madhubuti ya kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo ndio inayoongoza kwa idadi zaidi. Kwa mfano katika kipindi cha Julai- Desemba, 2023 OWMS ilipokea jumla ya notisi **529** za kusudio za kufungua mashauri. Kati ya notisi hizo Notisi **362** zaidi ya **asilimia 68** ya notisi hizo, zimetokana na migogoro ya ardhi.

Hivyo, kutambua kuwa masuala ya ardhi yanamgusa kila mwananchi, OWMS imeweka utaratibu kwa kushirikana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kushughulikia notisi hizo kwa kuhusisha taasisi husika ili kufanya majadiliano na wadai katika kipindi cha siku 90 za notisi za kusudio la kushitaki serikali. Pia OWMS imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake kuhusu masuala ya ardhi ili kuongeza ufanisi wa mawakili hao katika kushughulika mashauri ya ardhi kwa uweledi na kwa haraka zaidi.

**Ndugu Mgeni Rasmi**,

Kwa niaba ya OWMS napenda kuwahakikishia kuwa tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa weledi na uadilifu mkubwa na kutekeleza ipasavyo malengo ambayo kwayo ilianzishwa. Aidha, tunatambua

matarajio ya Serikali na Taasisi zake kwa OWMS, hivyo tunaahidi kuwa tutajitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu kuhakikisha tunatekeleza majukumu hayo na kufikia matarajio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.**

**Mhe. Mgeni Rasmi,**

Pamoja na mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa OWMS inakabiliwa na changamoto mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

i. **Usimamizi hafifu wa mradi au uwekezaji.** Suala hili hupelekea baadhi ya wawekezaji kutokutekeleza mradi kwa mujibu wa mpango wa uwekezaji (*investment plan*). Kwa upande mwingine, baadhi ya Wawekezaji, Watoa Huduma na Wakandarasi wanaopewa miradi ya kuendesha huwa hawana uwezo wa kutosha na hivyo kukwama katika utekelezaji. Na kutokana na usimamizi hafifu wa miradi hiyo, Wakandarasi/ wawekezaji hawa kukimbilia katika mabaraza pindi Serikali inapositisha mikataba/ miradi yao.

ii. **Ucheleweshwaji wa kufanyia kazi malalamiko ya Wawekezaji:** Katika baadhi ya kesi, Wawekezaji wamelalamika kuhusu mamlaka za Serikali kuandikiwa barua kadhaa za malalamiko mbalimbali. Hata

hivyo, mamlaka za Serikali zimekuwa hazitoi majibu kwa wakati na pengine hazijibu kabisa. Jambo hili lilisababisha wawekezaji kufungua mashauri kutokana na kukosa ushirikiano na majibu ya hoja mbalimbali.

iii. **Kutoshirikisha kikamilifu Ofisi ya Mwasheria Mkuu:** Baadhi ya Taasisi za Serikali kuvunja Mikataba bila kushirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hivyo kushindwa kufuata taratibu za kuvunja mikataba na kupelekea Serikali kushitakiwa katika Mahakama na Mabaraza ndani na nje ya nchi.

iv. **Kuchelewesha Malipo kwa Watoa Huduma na Wakandarasi:** Baadhi ya Taasisi za umma huchelewa kufanya malipo kwa wakandarasi na watoa huduma kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa bajeti iliyotengwa wakati Mkataba ulipoingiwa au kuchelewa tu kwa maamuzi ya malipo na hilo linasababisha Serikali kudaiwa deni, riba pamoja na gharama za kuendesha kesi.

**Ndugu Mgeni Rasmi;**

Pamoja na changamoto tajwa katika usimamizi wa mashauri, Pia ofisi hii inachangamozo zifuatazo kwenye masuala ya uendeshaji na utendaji kazi wa kila siku.

i. Ufinyu wa Bajeti umeendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Hali hii imesababisha kazi nyingi kutotekelezwa kutokana na kutokuwa na wigo mpana wa bajeti; Ukomo wa bajeti (budget ceiling). Bajeti haitoshelezi majukumu ya Ofisi mfano bajeti ya mafunzo ya maeneo ya ubobezi;

ii. Rasilimali watu iliyopo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ni ndogo, hivyo inaathiri utendaji kazi kwa kuwa mahitaji ya Ofisi kwa mujibu wa Ikama iliyopo kwa sasa ni Watumishi 312 (175 mawakili na 137 kada nyingine). Hivi sasa Ofisi ina upungufu wa mawakili **50** na watumishi **24** wa kada nyingine.

iii. Kukosekana kwa mawakili wenye ubobezi katika maeneo ya gesi, mafuta, uwekezaji, anga, madini, uchumi wa bluu, TEHAMA na maeneo mengine yakimkakati;

iv. Kukosekana kwa majengo ya Ofisi kwenye Ofisi za Mikoa inayotulazimu kupanga; na

v. Gharama za kuendesha mashauri ya nje ya nchi ni kubwa ukilinganisha na bajeti iliyotengwa jambo ambalo linasababisha kuomba kupatiwa fedha nje ya bajeti.

**OMBI MAALUM KWAKO MHE. MGENI RASMI**

OWMS inawasilisha ombi rasmi kwako na kukuomba uendeleze jitihada za kuisaidia OWMS katika kutatua changamoto zilizoainishwa hapo juu katika mambo yaliyo kwenye uwezo wako na yale ambayo unaendelea kuwa mwakilishi wetu kwenye mamlaka za juu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika Ofisi hii.

**Mhe. Mgeni Rasmi**

Kwa kumalizia, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko huu na kuja kutufungulia Kikao cha Pili cha Baraza la Pili la Wafanyakazi kwa Mwaka wa Fedha **2023/24**. Sanjari na shukrani hizo niwashukuru na kuwapongeza watumishi wote kwa maandalizi na kujitokeza katika Mkutano huu wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuwakumbusha kujadili masuala yote yatakayoletwa mbele yenu kwa weledi, hekima na busara ili Baraza hili liwe na tija.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa nikukaribishe Mheshimiwa Mgeni Rasmi ili uweze kuzungumza na wajumbe wa Baraza na hatimaye kutufungulia Kikao chetu.

**Asante sana kwa kunisikiliza.**